# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MBALATSE,
S.L. P 102,
MAKETE.
Barua pepe: mbalatsesecondaryschool@gmail.com
SIMU: 0768802800/0713462997
06/12/2022

Kumb.Na. MBS/FOS/1/VOL. 13
Mzazi/mlezi wa ________________________________________
S. L.P _____________________________

YAH**: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2023**

Hongera sana kwa kuchaguliwa kuja kusoma elimu ya sekondari katika shule ya sekondari Mbalatse. Shule hii ni ya hosteli kwa wanafunzi wote.

1. SARE YA SHULE

A. WASICHANA

(i) Suruali mbili (02) (rangi ya bluu bahari moja na rangi ya kaki moja)
(ii) Visolo viwili rangi nyeupe
(iii) Uje na viatu vyeusi jozi (pea) mbili vya kamba (gidamu) vyenye visigino.(viatu aina ya buti/raba haviruhusiwi)
(iv) Uje na sweta mbili damia ya mzee na pluu neki nyekundu kwa ajili ya kujikinga na baridi
(v) Uje na soksi jozi mbili nyeupe zisizo na maandishi au picha
(vi) Uje na vifaa vya kulalia; Godoro futi mbili na nusu kwa sita , blanketi zito, shuka mbili rangi ya bluu moja na pinki moja
(vii) Uje na vifaa vya michezo; raba na trakisuti nyeusi yenye miraba myeupe.
(viii) Uje na gauni ya damia mzee na tisheti ya bluu kwa ajili ya kuvaa baada ya masomo.
(ix) Uje na tranka kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyako
(x) Uje na vifaa vya kulia chakula ( kontena, kijiko)

.

B. WAVULANA

(i) Suruali mbili; rangi nyeusi moja na kaki moja.
(ii) Uje na suruali moja ya damia ya mzee na Tshirt ya kijivu yenye kola kwa ajili ya kuvaa baada ya masomo na pluneki nyekundu
(iii) Uje na shati mbili nyeupe za mikono mirefu (tomato/kangaroo)
(iv) Uje na viatu vyeusi jozi (pea) mbili vya kamba (gidamu) vyenye visigino vifupi (viatu aina ya buti/raba haviruhusiwi)
(v) Uje na sweta mbili damia ya mzee na pluu neki nyekundu kwa ajili ya kujikinga na baridi
(vi) Uje na vifaa vya michezo; raba na trakisuti nyeusi yenye miraba myeupe, bukta rangi yoyote.
(vii) Uje na soksi jozi (pea) mbili nyeusi
(viii) Uje na vifaa vya kulalia; Godoro futi mbili na nusu kwa sita , blanketi zito, shuka mbili; rangi ya bluu moja na pinki moja

ANGALIZO: HURUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI ZA AINA YOYOTE ILE

2. **VIFAA VYA USAFI**

A. WAVULANA

i. Uje na jembe jipya lenye mpini, kwanja moja, ndoo mbili za lita kumi na mfagio mmoja wenye mpini.

B. WASICHANA

ii. Uje na jembe jipya lenye mpini, kwanja moja, ndoo mbili za lita kumi na brashi kwa ajili ya usafi.

3. **VIFAA VYA KITAALUMA (KWA WOTE**)

a) Uje na rula ya 30cm
b) Uje na mkebe wenye vifaa vyote vya hesabu
c) Uje na madaftari makubwa (kaunta buku) kumi
d) Uje na kamusi (dictionary) kwa ajili ya kujifunzia lugha ya kiingereza
e) Uje na karatasi nyeupe (rimu A4 bunda moja) kwa ajili ya majaribio ya wiki kwa mwaka mzima.
f) Uje na mafaili mawili kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za kitaaluma

4. **MICHANGO INAYOTAKIWA KULETWA NA WAZAZI AU WALEZI WA MWANAFUNZI KWA MUJIBU WA MAKUBALIANO YA WAZAZI WENYEWE**.

**I.** Fedha ya chakula Tsh 100,000/=
**II.** Mahindi debe kumi (10)
**III.** Maharage debe tatu (03)

N.B michango hii utatoa kwa mchanganuo ufuatao:

| AINA YA MCHANGO | JANUARI-MACHI | APRILI-JUNI | JULAI-AGOSTI | SEPTEMBA-NOVEMBA |
|---|---|---|---|---|
| FEDHA | 25,000/= | 25,000/= | 25,000/= | 25,000/= |
| MAHINDI | DEBE 2 NA NUSU | DEBE 2 NA NUSU | DEBE 2 NA NUSU | DEBE 2 NA NUSU |
| MAHARAGE | LITA 15 | LITA 15 | LITA 15 | LITA 15 |

**FEDHA KWA AJILI YA CHAKULA LIPA KUPITIA BENKI AU NMB WAKALA HALAFU SHULENI UJE NA BPS ILI UWEZE KUPEWA RISITI. PIA UKUMBUKE KUANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE BPS.**

**N.B FEDHA TASLIMU HAITAPOKELEWA**

**NAMBA YA AKAUNTI NI 60410016936**

**JINA LA AKAUNTI MBALATSE SEKONDARY SCHOOL –CHAKULA**

**AINA YA BENKI NI NMB**

Fedha Tsh. 100,000/= (laki moja tu) ni kwa ajili ya kuwalipa wpishi, kununulia sukari, mafuta ya kupikia, chumvi, mchele, nyama, mafuta ya kusagia na kukobolea nafaka pamoja na kununua vifaa vya kupikia.

**ZINGATIA**

Kabla ya kufika shuleni hakikisha umekamilisha kujaza fomu namba 1, 2 na 3 kwa usahihi na uje nazo shuleni ambazo ni:

(a) Fomu namba 1 kukubali nafasi hii.
(b) Fomu namba 2 taarifa binafsi za mwanafunzi
(c) Fomu namba 3 ya kupima afya ya mwanafunzi kwa daktari ( hospitali na siyo zahanati)

***Ufikapo shuleni usikabidhi vitu vyako, na hasa kwa mwanafunzi yeyote ila kwa mwalimu anayehusika.***

**KUFUNGUA SHULE**

**Shule itafungua tarehe 09/01/2023 asubuhi.**

Mzazi/mlezi tafadhali mwandalie mwanao mahitaji yote, aje nayo shuleni ili kuondoa usumbufu kwa walimu.

NAKUTAKIA UTEKELAZAJI MWEMA

____________________________

ASINODI NAFTARI KIKOTH

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU NAMBA 1.

Mimi_______________________________________________________________________

Natokea Shule ya msingi__________________________________________nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Nimekubali kujiunga na jumuiya ya shule ya sekondari Mbalatse na nina ahidi kuwa mtiifu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za shule kama itakapoelekezwa.

Sahihi ya mwanafunzi________________________

Tarehe ___________________________

KWA MZAZI/MLEZI

Mimi __________________________________________

Kutoka (andika kitongoji na kijiji)___________________________________________________

S.L.P______________________________

Ambaye ni mzazi/mlezi wa_____________________________________________

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yalitolewa yahusuyo mtoto wangu nimekubali kuwa mwanangu aitumie nafasi hii.

Nina ahidi kumpa mahitaji yote na kushirikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza huyu kielimu na kitabia.

Ninaahidi kutoleta usumbufu kwa viongozi wa shule, wilaya, mkoa au wizara kwa kutaka kumhamisha mtoto wangu kwenda shule nyingine bila sababu ya msingi.

Sahihi ya mzazi/mlezi_________________________

Tarehe ______________________________________________

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU NAMBA 2. (MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI)

A.

1. Jina kamili la mwanafunzi___________________________________________________
2. Tarehe yakuzaliwa_________________________________________________________
3. Wilaya aliyozaliwa_______________________________________________________
4. Dini_____________________________________________________________________
5. Dhehebu__________________________________________________________________

B.

6. Jina la mzazi /mlezi anaye mtunza_____________________________________________
7. Kazi ya mzazi/mlezi_________________________________________________________
8. Anuani ya mzazi/mlezi_______________________________________________________
9. Namba ya simu_____________________________________________________________
10. Kata____________________________________________________________________

C.

11. Jina la mwenyekiti au katibu wa kijiji au kitongoji au mtaa__________________________
12. Kijiji/kitongoji_____________________________________________________________
13. S.L.P____________________________________________________________________
14. Namba ya simu____________________________________________________________
15. Mhuri wa ofisi ugongwe_____________________________________________________

D.

16. Jina la afisa mtendaji wa kijiji________________________________________________
17. Kijiji/kitongoji/mtaa_________________________________________________________
18. S.L.P____________________________________________________________________
19. Namba ya simu____________________________________________________________
20. Mhuri wa kijiji_____________________________________________________________

E.

21. Jina la afisa mtendaji kata___________________________________________________
22. Jina la kata________________________________________________________________
23. S.L.P_____________________________________________
24. Namba ya simu____________________________________
25. Mhuri wa kata _____________________________________

ZINGATIA: Tafadhali fomu hii ijazwe kwa usahihi.

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

FORM NUMBER 3:

MBALATSE SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 102,

**MAKETE.**

DATE_____________________________

Ref: NO.MBS/FOS/13

To the medical officer

To be completed by the medical in respect of all form one entrants and new school employers

Full name____________________________________________________________________

Age ________________________________________________________________________

Blood count (red and white)_____________________________________________________

Stool examination ____________________________________________________________

Urinalysis___________________________________________________________________

Syphilis test_________________________________________________________________

T.B. test ___________________________________________________________________

Eye test____________________________________________________________________

Ears test____________________________________________________________________

Abdomen___________________________________________________________________

Additional example physical defect of impairs infections chronically or family diseases Etc_____
_______________________________________________________________________________
I certify the above is cit/until to purse his/her lessons duties are required.
Signature ___________________________________________________________________
Desination__________________________________________________________________
Date_____________________________________station__________________________________________
NOTE

Medical officer: at the time of examination please treat the individual any ailments you note pupils employee. This completed form should be sent to the school with your acceptance of brought when you come to school

No student any Errol, any person and employed with ossification of physical fitness.

Delete as necessary.

## SHERIA ZA SHULE

1. Fika shueni  kwa kuzingatia ratiba iliyopo.
2. Fanya usafi eneo lako ulilopewa kabla ya vipindi kuanza
3. Hudhuria vipindi vyote vya shuleni kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa
4. Kuwa safi katika mawazo, maneno, vitendo na nguo
5. Ukiwa na shida au tatizo mwone mwalimu yeyote aliyekaribu nawe akusaidie vizuri na haraka zaidi
6. Uwapo shuleni hutarusiwa kubadili jina kinyume na sheria za nchi
7. Hutaruhusiwa kubadili dini uwapo shuleni mpaka idhini itolewe na mzazi/mlezi wako
8. Tabia ya kutoroka vipindi shuleni haita vumiliwa. Ukibainika utachukuliwa hatua za kinidhamu.
9. Utatakiwa kuwa na sare za shule muda wote uwapo shuleni
10. Utatakiwa kutii kengele na kuwahi kufika mahali panapotakiwa.
11. Ugomvi, matusi, na unyanyasaji wa aina yoyote haviruhusiwi kabisa.
12. Hauruhusiwi kuja na vazi la aina yoyote ambalo halijaorodheshwa kwenye aina ya sare za shule unazotakiwa kuja nazo ( ukurasa 1 na 2 hapo juu)

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE KWA MWANAFUNZI

1. wizi
2. uasherati na ushoga
3. ulevi
4. matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi cocaine, mirungi kubeli  n.k
5. kupigana au kupiga
6. kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. kudharau bendera ya taifa
8. kupata mimba au kusababisha mimba
9. kuoa/kuolewa
10. kutoa mimba
11. kugoma/kuchochea au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. kukataa adhabu
13. kuwa na simu ya mkononi
14. utoro wa vipindi
15. makosa yote ya jinai